# Changamoto Zinazowakumba wahusika wa Kiume Katika Riwaya za Kiswahili

Dorcas Kasiva Kimondiu, Esther Chomba na Francis Musyoka

Chuo Kikuu cha South Eastern Kenya.

Main Authors Email: d.kasiva2016@gmail.com

**IKISIRI**

Makala haya yanachambua changamoto zinazowakumba wahusika wa kiume katika riwaya ya Kiswahili. Mada hii ilichaguliwa kwa misingi kuwa suala la mwanamke limetafitiwa na watafiti wengi. Kukosekana kwa tafiti nyingi kuhusu jinsia ya kiume kumekuwa kukiathiri jamii kwa kuipa mitazamo kuwa jinsia ya kiume haikabiliwi na matatizo. Ili kufafanua changamoto zinazowakumba wahusika wa kiume, tutawarejelea waandishi mahuluti katika riwaya nne ambazo ni *Mwisho wa Kosa*, (1987) iliyoandikwa na Zainabu Burhani, *Siku Njema*, (1996) iliyoandikwa na Ken Walibora, *Taswira za Mawingu*, (2011) iliyoandikwa na Sinjiri Mukuba na *Nguu za Jadi,* (2021) iliyoandikwa na Clara Momanyi. Makala haya yanaegemea nadharia ya Mwanamume Mpya. Nadharia hii imetumika kueleza ni kwa nini baadhi ya wanaume hukaa na wake zao kwa usawa bila tabia za mfumo dume ambao huashiria kuwepo kwa taasubi ya kiume. Mbinu za utafiti zilizotumika ni usomaji wa riwaya teule kwa kina na uhakiki. Data iliyotumika katika makala haya ilitolewa maktabani. Maktabani, tasnifu, makala na vitabu vinavyohusiana na mada vilisomwa kwa kina. Uwasilishaji wa matokeo umefanyika kwa njia ya maelezo. Ni bayana kuwa utafiti huu utaifaa jamii ya wasomi wanaoshughulikia maswala ibuka katika jamii.

**Maneno Muhimu**: Kabili, Changamoto, Mhusika

**Utangulizi**

Makala haya yameangazia wahusika wa kiume katika riwaya teule za Kiswahili za waandishi wa kike na kiume. Riwaya za waandishi wa kike ni; *Mwisho wa Kosa* ya Zainabu Burhani na *Nguu za Jadi* ya Clara Momanyi. Riwaya za waandishi wa kiume ni; *Siku Njema* ya Ken Walibora na *Taswira za Mawingu* ya Sinjiri Mukuba. Wahusika ni viumbe wa kifasihi wanaoumbwa na mwandishi ili wawe sauti yake katika kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira (Muniu, 2011). Maoni yake yanashabihiana na ya Wamitila (2003) anayeeleza wahusika kama viumbe au watendaji wanaopatikana katika kazi ya fasihi. Wamitila (2008) anaibua hoja kuwa, maneno ya wahusika ni msingi mkubwa wa kuwakuza na kuwaendeleza hao hao wahusika. Kupitia kwa matendo na mazungumzo ya wahusika, wasomaji wanaweza kuzichanganua tabia zao.

Jamii mbalimbali zina mitazamo anuwai kuhusu wahusika wa kiume. Mwandishi hutokea katika jamii mahususi na kwa hivyo huweza kuwasuka wahusika wake kulingana na jamii alimokulia. Ken Walibora, Zainabu Burhani, Sinjiri Mukuba na Clara Momanyi ni wanajamii waliokulia katika jamii zao na tunaamini kuwa wamewasawiri wahusika wa kiume kwa mujibu wa jamii zao.

Jamii huchukulia kuwa mtoto wa kiume anajiweza na hivyo hahitaji kulindwa (Wizara ya Elimu, 2014). Suala hili likichukuliwa kwa uzito mtoto wa kiume ataangamia. Vilevile kule kumweka pembeni kunaweza kupelekea kujiingiza katika vitendo vya uhalifu. Wazo hili limetiliwa uzito na Hamisi, (2018) anapodai kuwa mtoto wa kiume asiposhughulikiwa ataathirika kama vifaru weupe barani Afrika. Jambo ambalo litampelekea kujiingiza katika kufanya vitendo vya uhalifu.

Usawiri wa kijinsia umetafitiwa katika nyuga mbalimbali, kama vile elimu, ajira, malezi, afya, siasa, utamaduni, uchumi, fasihi na pia kwenye mitandao ya kijamii. Tangu kuanza kwa mawazo ya Ufeministi ulimwenguni, imekuwa

ikijadiliwa ni namna gani wanawake wanaweza kujikomboa kutoka katika ufungwa wa mwanamume na kupata haki na wajibu sawa. Pamoja na hatua kubwa iliyopigwa, mapigano haya hayawezi kufanikiwa iwapo yatakuwa mapigano ya wanawake dhidi ya wanaume. Iwapo mwanamume ataachwa nyuma na asikombolewe kutoka katika ufungwa wa kifikra, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni, mapambano haya hayatafanikiwa (Badru, 2019). Fasihi ina mchango mkubwa katika mapambano haya ya ukombozi wa mtoto wa kiume dhidi ya mfumo dume.

**Nadharia ya Mwanaume Mpya**

Nadharia hii iliasisiwa na Beynon (2002) ambapo alifafanua kuwa mwanamume sio mbabe nyakati zote na kwa kila jamii bali wapo wanaume ambao wanajali sana, wasikivu na wanaotii maagizo ya kiuana. Kuna wanaume ambao muonekano ni wapole sana ila wanatawaliwa na mfumo dume.

Kwa maana hiyo jamii ina wanaume mchanganyiko wakiwemo wanaume wapya yaani walioondokana na mfumo dume na ambao wanaushikilia. Nadharia hii inalenga kuwaonesha wanaume wapya ambao wamebadilika na kuwa katika utendaji mpya ikilinganishwa na mfumo uliotekelezwa na wanaume awali. Mikondo mbalimbali ya uanaume inategemea elimu rasmi, vyombo vya mawasiliano na utamaduni wa Kimagharibi. Kwa mfano, wanaume wanaobadilika kuusheheni upya wa tabia wanakubali majukumu yoyote ya kiuana kwa kutojali jinsia, hawaonyeshi udikteta na wanawajibika katika kufanya majukumu ya kinyumbani. Pamoja na haya wanaweza kuzikosa nafasi zao na mazoea yao (Morell, 2002).

Wanaume wapya huwasaidia wake zao kujiendeleza kielimu na kikazi. Vilevile, wanaweza kufanya kazi za jikoni kama kuosha vyombo na kulinda watoto bila kuogopa kuwa watafanyiwa masihara na wanaume wenzao au jamaa walioko karibu nao. Kulingana na Gill, (2003) mwanaume mpya ana hisia chanya, anawaheshimu wanawake na anawaona wanaume kwa wanawake kuwa viumbe sawa. Ni mtu anayejipenda kwa kuzingatia jinsi hulka yake ilivyo. Ana hisia za kike za kulinda watoto kama baba mwema.

Nadharia hii inaungwa mkono na Newman, (2012) ambapo ameeleza kuhusu mtazamo huu mpya wa uana kuhusu mwanaume wa kisasa au anayetarajiwa kuwa wa kisasa kwa kumsaidia mkewe kama kiumbe sawa. Mkondo huu umesaidia kumchanganua mwanaume anayeelekea kuwa chanya kwa mwanamke tofauti na wanaume walio wengi katika jamii za Kenya na Afrika kama ilivyobainishwa na waandishi.

**5.2 Changamoto Zinazomkabili Mhusika wa Kiume**

Mhusika wa kiume katika jamii hukumbana na changamoto mbalimbali katika maisha zikiwemo za kifikra, kiuchumi, kisiasa na kijamii. Hata hivyo, imebainika kuwa wengi wao huchelea kufichua matatizo yao kwa wenzao kazini au watu wa familia zao. Wanajamii wanastahili kuwapa wanaume mazingira salama ya afya za akili ili waweza kufungua mioyo yao kwa wengine. Jamii ya sasa inaelekeza nguvu zaidi kwa mtoto wa kike na kumsahau mtoto wa kiume. Jambo hili huenda likawa na madhara ya baadaye katika jamii zetu.

**5.2 Dhuluma Kutoka kwa Jamii na Walezi**

Dhuluma ni hali ya kutokipa kiumbe haki yake au kukitesa kimwili au kisaikolojia. Kiumbe kinapodhulumiwa, huenda kikafikia maamuzi mazito au kutamauka maishani. Dhuluma miongoni mwa wanajamii sio jambo geni. Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, kuna baadhi ya wazazi wa kiume kama vile Sagilu wanaowatumia wanao wa kiume kama vyombo vya kuendeleza uovu katika jamii. Wazazi hao wa kiume wanaongozwa na taasubi ya kiume. Hawaelekezi wavulana wao kwa njia inayofaa. Haya yanadhihirika katika nukuu ifuatayo:

> Mashauri alianza kusimulia tokea mbali. Huku machozi yakimtiririka, aliwaambia jinsi Mzee Sagilu alivyomtumia mara kadha kumhasi Lonaro. Alisimulia jinsi alivyoshauriwa na Mtemi kubomoa jengo la Lonare kwa sababu ya husuda tu. Alisimulia mengi maovu aliyotenda kwa niaba ya babake. Wote walimsikiliza kwa hamu. Wakasalia kutoa vimako mara kwa mara. (uk. 126)

Kutokana na nukuu hii, mhusika Sagilu anadhihirisha kuwa kiongozi na mlezi mbaya wa mtoto wake wa kiume (Mashauri). Sagilu anamkandamiza mwanawe kimaadili. Badala ya kumwelekeza kuwa mvulana anayewajibika kimaadili katika ujenzi wa jamii yake, anamfundisha kuwa katili na mbinafsi asiyejali mali ya watu wengine. Mashauri anaonekana kufuata ushauri wa baba yake Sagilu. Anamhujumu Lonare kwa kubomoa jengo lake.

Katika riwaya ya *Siku Njema*, suala la dhuluma limejitokeza kupitia maisha ya Kongowea Mswahili. Baada ya kifo cha mama yake Zainabu Makame, aliachwa mikononi mwa mjomba wake Kitwana. Mwanasaumu mkewe mjomba alimdhulumu kwa njia mbalimbali. Mwandishi anaeleza haya kupitia dondoo hii:

> Mwanasaumu alinitendea madhila yasiyokuwa na mfano. Nilikula makombo wakati mwingine na kutendeshwa kazi zisizo na kikomo. Nilipaswa kufagia nyumba, kupiga deki, kupika, kupakua, kufua nguo, kuzipiga pasi, kukuna nazi kwa mbuzi na kazi nyinginezo. Binamu zangu walikuwa wakikaa tu raha mustarehe wameandika nne kwa miguu yao au wanabukua vitabu (uk. 23).

Kupitia maelezo haya, ni bayana kuwa Kongowea alipitia mateso mengi. Mwanasaumu hamjali Kongowea. Ingawa ni mtoto mdogo, anamfanyisha kazi nyingi bila kujali umri wake. Kazi hizo zinamkosesha wakati wa kusoma. Kongowea alivumilia kwani hakuwa na mahali pengine pa kwenda wala mtu mwingine wa kumtegemea. Dhana hii inafafanua kuwa wanajamii wana jukumu la kuwasaidia watoto ambao wana shida mbalimbali.

Katika riwaya ya *Taswira za Mawingu*, Kulesoni alipitia madhila mengi mikononi mwa mama wa kambo. Mwendi alikuwa akimtesa Kulesoni huku akiwapendelea wanawe. Alimfanyisha kazi ngumu bila kujali hali yake ya kiafya. Alimyima chakula. Haya yanabainika kupitia nukuu hii:

> Basi baada ya ugomvi mkali Kulesoni akapokea amri ya kuelekea kichakani kutafuta kuni. Giza lilikuwa limeshaanza kuingia na uoni ungemwia yeyote vigumu, hata mwenye ukoo wa damu ya paka. Kulesoni alikuwa akiumwa na jino, aliumwa vibaya la sivyo angetafuta kuni mchana. Lilikuwa limemwanza saa nne asubuhi hivi. Hata hivyo alipoingia kichakani, giza lililoanza kuingia, rasharasha za mvua zilizoanza kupapata pamoja na mapigo ya maumivu ya jino iliyomchimba hadi kichwani, vilimzuia kuona chochote barabara. Basi aliukanyaga mwiba mkubwa uliomwingia mguuni sawasawa. (uk 3)

Kulesoni kama watoto wengine mayatima anapitia mateso mengi mikononi mwa mama wa kambo. Anatumwa kutafuta kuni wakati wa usiku. Alikuwa anaumwa na jino. Kule kutembea gizani kunamfanya kudungwa na mwiba. Hakuwa na pengine pa kuita nyumbani ila kwa huyu tu mama wa kambo. Watoto wengi hukumbana na hali ngumu ya maisha chini ya welezi wao.

Katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa*, mhusika wa kiume Rashid alidhulumiwa kikazi. Bwana Matata alipobaini kuwa Rashid alikuwa kikwazo kati yake na Monika, alipanga njama ya kumdhulumu kikazi. Rashid alikuwa mfanyikazi wa kutegemewa katika ofisi ya Salimu. Alifanya kazi kwa kujitolea. Matata alikuwa ameamua kumdhulumu Rashid kikazi. Alimshawishi Salimu hadi akakubali ombi la kumwondoa Rashid kazini. Nukuu hii ya mazungumzo kati ya Salim na Matata inafafanua haya:

> “Sikiliza”, alimkatiza Matata, “kesho ukitaka nitakuletea mtu mwengine aliye hodari kuliko yeye.” “Siyo muhimu angalau uniambie amefanya nini?” “Nimekuambia. Anajiona sana. Anajidai kuingilia katika mambo yasiyomhusu. “Mambo kama yepi? Ah, lakini huna haja ya kunieleza. Wafikiri nitaelewa.” “Ehe, ndiyo hivyo mwenzangu. Hata mimi siulizi mengi,” (uk. 195).

Rashid anadhulumiwa kwa sababu ya uhusiano wake na Monika. Alikuwa mfanyakazi mwema lakini tamaa ya Bwana Matata ikamfanya kufutwa kazi. Matata alikuwa na wazo kuwa Rashid aliingilia penzi lake na Monika.

**5.3 Hali Ngumu ya Maisha**

Katika maisha, changamoto na hali ngumu ya maisha ni sehemu isiyoepukika. Changamoto kubwa ni jinsi ya kuhimili matatizo yanayowakumba wanajamii katika maisha. Kama mwanadamu yeyote, mwanamume hukabiliwa na changamoto si haba. Katika ulimwengu wa sasa kuna mabadiliko chungu nzima duniani yanayosababishwa na masuala anuwai kama vile maendeleo ya kiteknolojia na utandawazi.

Kutokana na hali ngumu ya maisha, mwanamume anatumika kama chumo na mwanamke. Wanawake hutumia njia hii kujinufaisha. Wanapata pesa kutoka kwa wanaume na malipo ni miili yao. Kavuria, (2008) anaeleza kuwa mtu huweza kukumbwa na hali ngumu ya maisha na ashindwapo kuisuluhisha huweza kukata tamaa. Mawazo ya Kavuria yanatoa mwanga kuhusu hawa wanawake waliokata tamaa.

Kule kutumika kwa mwanamume kama chumo ni mmomonyoko wa maadili. Maadili ni mienendo au tabia njema inayokubalika katika jamii mahususi, kama sehemu ya maisha ya jamii husika (Watuha, 2011). Mmomonyoko wa maadili ni hali ya kukiuka maadili fulani (Waeni, 2023). Kgatia, (2013) anasema kuwa, kupitia vyombo vya habari na burudani kwa mfano televisheni, simu tamba, redio, mtandao, magazeti, filamu na video, utamaduni wa magharibi umesambazwa kote ulimwenguni. Utamaduni huu wa magharibi, umeenea kote Afrika kupitia utandawazi na umeathiri sana maadili na amali za Kiafrika.

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, kuna wanawake ambao utashi wao wa maisha ya anasa na pesa unasababisha ukandamizaji wa mwanamume. Wanawake hao wanachohitaji ni pesa si penzi la dhati. Haya yanabainika katika nukuu hii:

> *I say,* wajua nimewaona wapi leo? Katika hoteli ya *Saturn.* Cheiya na Sagilu wameshikana. "Sasa umeamini au sivyo." "*Don't joke with some of these modern girls my friend. Their thirst for money is unquenchable."* Mashauri aliketi na kushusha pumzi. (uk. 178)

Kutokana na kauli hii, mhusika mwanamke amesawiriwa kama kiumbe asiye na mapenzi ya dhati na aliyebeba ushawishi na tamaa zote za ulimwengu. Nukuu hii inaonesha mwanamke kama mtegemezi wa mwanamume. Mwanamume anapotumiwa kama chombo cha kukidhi mahitaji ya mwanamke, yeye huchukulia ni jukumu lake kama vile anavyotarajiwa na jamii yake (Waeni, 2023). Mwanamke Cheiya ametumika kusambaratisha uhusiano mwema kati ya baba mzazi na mwanawe na kuzua uhasama baina yao. Mawazo ya Reynolds, (2020) yanaugwa mkono na kisa hiki ambapo kwenye Biblia Takatifu, mwanamke aliyeumbiwa Adamu alishikwa na tamaa za ulimwengu zilizofifisha uhusiano mzuri kati ya Adamu na Mungu.

Mwanamke anastahili kujua kuwa hata kama nyakati za maisha ni ngumu, kuna njia mbadala mbalimbali za kujikimu kimaisha kama vile ususi, ushoni, kilimo na hata mamantilie (Kimondiu, 2019). Anaendelea kusema kuwa, kujihusisha na kitendo cha ngono siyo suluhisho la hali ngumu ya maisha. Wanaume wanastahili kubadilika na kuwa wapya. Wanaume wapya huzielewa mbinu wanazotumia wanawake kuwachuma. Mwanamke hupata starehe kwa gharama za mwanamume.

Kwenye riwaya ya *Siku Njema*, mwanamke anamtumia mwanamume kama chumo. Kongowea alikutana na Amina chomboni. Amina alimlipia Kongowea nauli alipopoteza pesa. Waliandamana hadi kwa Amina. Kongowea alipokaribishwa na Amina nyumbani kwake alikuwa na maswali mengi kichwani. Alitaka kujua walichofanya wanawake aliowaona mtaani wamevalia mavazi haba na kuketi kwenye stuli milangoni. Wanawake wale waliwakonyezea macho na kuwavutia wanaume wapitao. Amina anaeleza haya kupitia nukuu hii:

> "Si wamo katika kuzubua riziki yakhe?" alijibu. "Hiyo ndiyo riziki walioandikiwa. Hapa duniani hakuna kazi mbaya. Kwani hujasikia msemo *kazi mbi si mchezo mwema."* "Wanafanya kazi gani hawa?" nikauliza kwa umbea. "Usijitie hamnazo Mswahili. Hawa wenzangu wako kwenye chumo bwana, ushaona? Biashara ya nipe nikupe katika ulimwengu huu wa toa na twaa. Si hoja kama biashara ni haramu au halali: hoja ni kama muuzaji na mnunuzi wameridhiana." (uk. 54)

Wanawake hawa hawajali kama wanachofanya ni kizuri au kibaya haja ni wapate pesa. Maneno haya yanadhihirika pale Amina aliposema kuwa, sio hoja kama biashara ni haramu au halali. Wanaume wanatumika na wanawake hawa kama kitega uchumi. Wanapofanya kazi zao, pesa wanazopata wanazileta kwa wanawake hawa. Biashara ya aina hii inaweza kueneza magonjwa ya zinaa kama vile UKIMWI. Vilivile, watoto haramu hupatikana kupitia njia hii. Wanawake wengine huavya mimba na jambo hili linaweza kusababisha kifo cha mhusika.

Matei, (2011) anasema, dhima mojawapo ya fasihi ni kuadilisha. Matendo mema huhimizwa na mabaya hukashifiwa kwa kuadhibiwa kwa mhusika hasidi. Japo wanawake hawa wanatenda tendo lisilo la kimaadili, hii ni hali halisi katika jamii ya sasa kwani fasihi inafungamana sana na mitindo ya maisha ya kila siku. Maudhui yake yanagubika kipengele cha maisha ya binadamu. Uasherati waelekea kuonekana kama jambo la kawaida duniani. Wanaume wanastahili kujirudi na kuachana na mienendo ya aina hii kwani wao ndio huchangia pakubwa na hatimaye wanapoteza.

Katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa*, mhusika wa kiume Bwana Matata anatumika kama chumo na Monika. Wakati wote Monika aliona fahari kuonekana na Matata kwa sababu ya cheo chake na hata gari lake la kifahari. Monika alinunuliwa nyumba na Bwana Matata waziri wa Elimu. Monika alifurahi sana alipoupata ufunguo wa nyumba yake. Mwandishi anaeleza:

> Alipoifungua, alitoa karatasi iliyokunjwa na alipoinyosha aliona ufunguo umebandikwa kwenye karatasi ile kwa karatasi ya gundi, na maneno kidogo yameandikwa. Ile nyumba sasa tayari na huu ndio ufunguo wa mlango wa nje. (uk. 199)

Monika kama wanawake wengine walio na tamaa ya pesa na mali alipenda kuchuma kwa wanaume. Alinunuliwa nyumba na Bwana Matata, alipenda kujihusisha na wanaume wenye pesa na vyeo vya hadhi. Bwana Matata alikuwa akifikiria kuwa Rashid alikuwa mchumba wake Monika kwani waliishi katika nyumba moja. Aliamua kutumia cheo chake kumtesa Rashid. Ni bayana kuwa, wanaume wengine kwenye jamii huathirika kutokana na tabia hii ya kuchuma. Walio na nguvu na vyeo vya juu, huwadhulumu wanaume wenye vyeo vya chini mradi wapate wanachotaka. Hii ni changamoto kwa mhusika wa kiume kwa sababu mwanamke humtumia kujinufaisha yeye mwenyewe.

Hali hii ya kukidhi mahitaji kwa sasa imekuwa kisingizio kikubwa kwa wanawake walio wengi (Fakih, 2017). Fakih anaeleza kwamba, biashara hii ya danguro na ukahaba ni tabia mbaya inayowafanya baadhi ya wanawake kujishughulisha katika kuuza miili yao kwa wanaume ili kukidhi mahitaji yao. Tabia hii kwa kawaida inaleta athari za kiafya, sio tu kwa mwanamke peke yake bali pia kwa mwanamume. Ni vyema kwa wanajamii kuachana na tabia za aina hii na mwanamke mwenyewe kutambua thamani yake na kutokuwa tayari kutumika kama bidhaa kwa wanaume.

Kutokana na mamlaka yake Bwana Matata, anamkandamiza Rashid. Alimuona kama kizuizi cha kumpata Monika. Mutungi (2008), anaeleza kuwa, wanaume ambao wana mamlaka na nguvu nyingi wanawakandamiza wanaume wasio wababe. Rashid anateseka kwani hakuwa na uwezo na mamlaka kama Bwana Matata. Matata anasababisha kufutwa kazi kwa Rashid kwa sababu ya Monika. Ni bayana kuwa wapo wanaume wengi katika jamii ambao huteseka kutokana na wanawake kuchuma.

**5.4 Kukosa Kuendelea na Masomo**

Kukosa kuendelea na masomo ni kukosa kukamilisha kipindi cha masomo kutokana na aidha ulitima miongoni mwa wazazi, utoro wa wanafunzi au sababu nyingine. Vijana wanaomaliza masomo yao kwa ngazi mbalimali za elimu, wengi wanakosa nafasi ya kuendelea na masomo yao kwa sababu ya mfumo rasmi wa elimu (Bwaya, 2017). Mara nyingi vijana hukosa kuendelea na masomo kwa sababu ya kukosa ufadhili wa masomo yao au uwezo wa chini wa wazazi wao. Vijana wengi hutamauka na baadhi yao kulazimika kurudi mitaani kutafuta namna ya kuendesha maisha yao.

Katika riwaya ya *Taswira za Mawingu*, Kulesoni alikumbana na matatizo si haba katika kipindi chake cha elimu. Alipohitimu darasa la nane, alitarajia kuendelea na masomo yake. Baba yake Matuta alikuwa mlevi. Siku moja Kulesoni alimwamsha akitaka kujua hatima ya masomo yake. Mwandishi anaeleza haya katika nukuu hii:

> "Baba! Baba! Baba sasa umesemaje kuhusu elimu yangu ya shule ya upili? Maana naona siku zinakatika. Nimekutana na wenzangu kadhaa wameshanunuliwa masanduku na vifaa kadhaa wanavyohitaji tayari kwenda shuleni "Sitaki kusumbuliwa na mambo mengi." Sauti ya baba yake ilitoka ndani. (uk 125)

Kupitia nukuu hii ni wazi kwamba Kulesoni alikuwa na matarajio makubwa ya kuendelea na elimu. Baba yake anamvunja moyo kwa maneno aliyosema. Kule kukosa makubaliano mema kati ya baba na mwana, kulimfanya Kulesoni kumwibia baba yake pesa ili aweze kujiendeleza kielimu. Alipitia changamoto nyingi katika kusaka elimu. Hatimaye alifanikiwa kujiunga na chuo kikuu japo kwa shida nyinyi.

Vilevile, katika riwaya ya *Taswira za Mawingu* mhusika wa kiume Zingwi hakukamilisha masomo yake. Zingwi hakuwa mwerevu darasani. Masomo yalimwia magumu. Hakujua kuandika hadi siku moja aliponakili jina la msichana mwingine darasani kwenye uandishi wa insha. Mwandishi anaeleza haya:

> Zingwi alikuwa kijana mwenye umri wa miaka kumi na minane hivi. Alikuwa mtu mnyamavu na mwenye bidii na ari shambani lakini mambo yalimwia mazito sana masomoni. Kiwango cha juu zaidi alichowahi kutimia ni darasa la sita kabla ya kulemewa kabisa na kuamua kukaa nyumbani baada ya wazazi na walimu kusalimu amri. (uk. 114)

Maelezo ya nukuu hii yanaeleza jinsi walimu na mfumo rasmi wa elimu ulivyochangia kutokamilisha shule kwa mhusika huyu wa kiume. Kule kusoma insha ya mwanafunzi darasani mbele ya wanafunzi wenzake kulimvunja moyo. Alinakili jina la Rosmary Yondo na kuliandika kama jina lake badala ya Zingwi Mena.

Alipoacha shule na kwenda kukaa nyumbani, nukuu inaeleza kuwa alikuwa na bidii na ari shambani. Zingwi kwa sababu ya kukaa nyumbani mawazo maovu ya ubakaji yalimjia akilini. Alijaribu kumbaka mpwa wake Monii. Monii alikuwa mtoto mdogo hata asijue alichotarajia kumfanyia mjomba wake. Kitendo hiki kilimfanya Monii kumwogopa mjomba wake asimkaribie tena maishani.

Walimu huwa na uhusiano wa moja kwa moja na wanafunzi wanapokuwa shuleni. Walimu wana jukumu la kuwasaidia watoto wakue wakijiamini na kujipenda (Taasoni, 2002). Wakosapo wanatarajiwa kuwaelekeza kwa njia ya kuwatia moyo. Baadhi ya walimu huwavunja moyo wanafunzi wao. Mwalimu wa Zingwi angemwelekeza vyema angekamilisha masomo yake. Mfumo wa elimu nao unawahujumu wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Nchini Kenya mfumo mpya wa umahiri (CBE) ulioanzishwa mnamo Desemba 2017 ni mfumo unaozingatia maendeleo ya kila mwanafunzi. Mfumo huu unahakikisha wanafunzi wanamaliza masomo wakiwa na ujuzi unaohitajika kwenye soko la ajira au maisha halisi. Abuya (2017) anaeleza kuwa Mtaala wa Umahiri umeweka mahitaji ya mtoto mbele ya yale ya shule, mwalimu na mzazi. Lengo la mtaala huu ni kuhakikisha kuwa maarifa

ambayo mwanafunzi amepeta shuleni anayatumia kutekelaza shughuli mbalimbali katika mazingira yake halisi anamokulia kila siku.

Badala ya kusoma kwa ajili ya mtihani, mwanafunzi anajifunza ili kutatua matatizo halisi na kuwa tayari kwa kazi au kuanzisha miradi yake binafsi. Zingwi alikuwa hodari shambani, kwa hivyo mfumo wa elimu ulimfanya kutotimiza ndoto yake ya kuwa mkulima hodari. Wengi wa wanafunzi hukumbana na changamoto za aina hii kupitia mfumo na walimu wasiowaelekeza vizuri. Wanafunzi hawa hukosa kukamilisha kipindi chao cha elimu na mwishowe huingilia tabia zinazokiuka maadili ya jamii.

Kukosa kuendelea na elimu miongoni mwa mhusika wa kiume kunajitokeza katika riwaya ya *Nguu za Jadi.* Mangwasha anaoneka kuumia moyo kila anapowaona vijana wale wa kiume wakijikusanya kwenye viambaza vya maduka bila kufanya lolote. Mwandishi anaeleza:

> Mangwasha aliungulika moyo alipokuwa akiwaona vijana hasa wa kiume wamejikusanya kwenye viambaza vya maduka. Hawakuwa na shughuli maalumu iliyowakutanisha pale ila kulisukuma gumzo tu. Wengi walikuwa wamemaliza shule kidato cha nne au darasa la nane. Lakini kutokana na hali ngumu ya maisha ya wazazi wao, vijana hao hawakuendeleza elimu yao. Huo ukawa mwisho wao wa kubukua mabuku. Wengine walizurura tu katika baraste za miji wasijue wafanyalo. (uk. 48).

Kutokana na maelezo haya, ni dhahiri kuwa mhusika wa kiume anapokosa kukamilisha masomo yake hukosa la kufanya. Vijana hawa wa kiume wanaonekana kujikusanya kwenye viambaza vya maduka. Hawafanyi lolote. Wengi walikuwa wamekamilisha kidato cha nne na wengine darasa la nane. Hawa ni vijana ambao hawana ujuzi wowote wa kujiendeleza. Wengine wanaonekana kuzurura tu katika barabara za miji wasijue wafanyalo.

Kukosa kuendelea na elimu, humdumaza mwanadamu na kumfungia nafasi za kujiendeleza maishani. Uger, (2007) anaeleza kuwa watoto wengi wa kiume nchini Kenya hukumbana na changamoto nyingi katika maisha yao ya shuleni na hawakamilishi masomo ya sekondari ipasavyo. Anaeleza kuwa hata wale wanaomaliza masomo ya sekondari ni wachache ambao hujiunga na vyuo vikuu ama vya kiufundi. Utafiti huu umekubaliana na mawazo ya Uger kwa sababu katika jamii wapo vijana wa kiume ambao wanakosa kukamilisha masomo yao na wako mitaani tu bila kazi.

Momanyi anawatambua vijana wa kiume katika kizazi cha leo. Vijana hawa huamka na kwenda sokoni. Wanakusanyika katika maeneo ya maduka. Wengine wanazurura barabarani wasijue la kufanya. Kule kukosa la kufanya, mwishowe huwafanya wale vijana wa kiume kujiingiza kwenye vitendo vya uhalifu na utumiaji wa dawa za kulevya.

Katika riwaya ya *Siku Njema*, mhusika wa kiume Kongowea Mswahili hakuweza kukamilisha masomo yake. Hili lilitokana na kifo cha mamake Zainabu Makame. Kongowea alibaki mikononi mwa mjomba wake, ambaye alikuwa mgonjwa wakati alipoufanya mtihani wa kitaifa. Kongowea alipokea barua ya kujiunga na shule ya upili lakini haya hayakuwa. Nukuu hii inaeleza haya:

> Siku chache baadaye nilipokea barua ya kuniita katika shule ya upili ya kitaifa Buguruni, Dar es Salaam. Lakini ndoto yangu ya kusoma hadi chuo kikuu nihitimu ama udakitari au urubani haikuweza kutimia kamwe. Mjomba Kitwana alikuwa na nia ya kunilipia karo, lakini maradhi ya mkono yalimaliza pesa zake zote katika kujaribu kuyaganga. (uk.27)

Nukuu hii inaeleza vile Kongowea alivyokuwa na kiu ya kuendelea na masomo ili kutimiza ndoto yake. Haya hayakuwezekana kutokana na ugonjwa wa mjomba wake. Mhusika huyu anaeleza vile mjomba wake alivyokuwa na nia ya kumlipia karo lakini hakuwa na uwezo. Mamake mzazi alikuwa ameaga dunia naye mkewe mjomba alikuwa katili. Mhusika huyu akabaki bila wa kumuauni.

Kulingana na Hong, (2019) baadhi ya wavulana wanaoachwa mayatima au bila walezi hawaendelei na elimu yao. Anazidi kueleza kuwa wavulana hao hupata changamoto ya kifedha jambo ambalo huwafanya watafute kazi ili wakidhi mahitaji yao. Mawazo ya mtafiti huyu yanaungwa mkono na utafiti huu kwani mhusika Kongowea alikosa kuendelea na masomo yake baada ya kifo cha mama yake. Alipopoteza nafasi yake ya kujiunga na shule ya Buguruni, Dar es Salaam, Kongowea alianza kufanya kazi za vibarua ili kukidhi mahitaji yake. Hii ni hali halisi ya vijana wa kiume wanaokosa kukamilisha elimu yao katika jamii.

Mfanyakazi aliyeitwa John Amon katika riwaya ya *Siku Njema* hakuweza kukamilisha elimu yake. Wazazi wake walishindwa kumlipia karo kutokana na umaskini. Mwandishi anaeleza haya:

> John Amon alikuwa ghulamu Mtrukana mwenye jadi ya kimaskini. Aliwahi kwenda shule mpaka darasa la sita naye alikuwa shujaa. Lakini mama mfaruku akashindwa kumlipia karo ya shule. Maskini akalazimika kuacha shule na kutafuta kazi ya uchungaji katika mashamba ya wakwasi. (uk. 116)

Kutokana na nukuu hii, ni bayana kuwa John alikuwa na hamu ya kusoma. Umaskini na kifo cha baba yake, ulichangia kukatiza masomo kwake. Baada ya kukatiza masomo aliingilia kazi duni ili kukidhi mahitaji yake. Alikuwa mchungaji katika shamba la mzungu mmoja aliyeitwa Patrick MacDonald.

Selemani Mapunda ni kijana wa kiume katika riwaya ya *Siku Njema*. Alitoroka shuleni alipoamrishwa na mwalimu mkuu aoge mbele ya kaumu ya wanafunzi. Inasemekana kuoga kwake kulikuwa nadra sana. Alikuwa na mnuko mithili ya beberu. Alipovua shati na wanafunzi wenzake kuanza kumcheka aliamua kutoroka. Hiyo ikawa ndio siku yake ya mwisho shuleni. Mwandishi anaeleza haya:

> Alipotoroka shuleni, Selemani akawa lofa aliyezurura ovyo ovyo mjini Tanga. Akajiunga na genge la vijana wengine waliozuumu kutenda kila amali mbaya. Akaanza kuvuta bangi na kuiba mali za watu, sikwambii kunajisi mabinti za watu. (uk.20)

Kutokana na maelezo ya nukuu hii, ni wazi kuwa vijana wa kiume wanapokosa kukamilisha masomo yao hujiingiza kwenye vitendo vya uhalifu. Hatima ya uhalifu huu ni jela au kifo. Mwalimu mkuu alichangia pakubwa kuacha shule kwa Selemani. Taswira hii ya Selemani kuacha shule imetumika kwenye nukuu hii ili kuibua uzito wa matatizo wanayopitia wanafunzi wa kiume mikononi mwa walimu. Ndoto zao hukatika ghafla kwa sababu ya utoro.

Katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa,* mhusika wa kiume Ali hakuweza kukamilisha masomo yake ya chuo kikuu. Ali alikuwa mwanafunzi hodari. Aliuziwa dawa za kulevya ili aweze kuongeza uwezo wake wa kusomea mtihani. Alikosa usingizi akisomea mtihani. Hali yake ya afya iliathirika baada ya kutumia vidonge vile. Usimamizi wa chuo ulipobaini ukweli kuhusu hali ya Ali, uliamua kumsimamisha asiendelee na masomo. Nukuu hii ya barua aliyopokea inaeleza haya:

> *Bwana Ali Bushiri,*
> *Baada ya majadiliano, Baraza la Chuo Kikuu limeamua kuwa halitaweza kukupokea katika mwaka ujao wa masomo kama mwanafunzi wa chuo hiki ilivyokuwa umevunja sheria za chuo baada ya kuarifiwa sheria hizo. Tunakuombea mafanikio katika maisha yako ya mbeleni.Mkuu wa Shughuli za Wanafunzi.*

Ali aliyatarajia haya kwani alielewa sheria za chuo. Uchungu wake ulikuwa mwingi. Kule kutopokelewa tena kama mwanafunzi, kulimlazimu kujiangalia kama mtu mzima bali si mwanafunzi. Alilazimika kutafuta njia ya kujiendeshea maisha yake. Wazazi wake hawakuwa na uwezo wa kumpeleka nchi za nje kwa masomo kwa hivyo hakuona haya ya kuzungumza nao. Ali alikuwa na hamu ya kuendelea na masomo. Hatimaye Ali aliamua kutafuta kazi. Alikuwa akifanya kazi masaa mengi kwa pesa kidogo.

Suala la dawa za kulevya limekuwa ni kero katika jamii kutokana na athari zake hasi. Kulingana na ripoti ya NACADA (2016), mazingira ya shule za upili ni eneo mojawapo ambalo vijana hutumia dawa za kulevya. Utafiti huu unakubaliana na mawazo ya ripoti hii kwa sababu mhusika Ali aliuziwa dawa za kulevya katika eneo la chuo kikuu. Kwa hivyo, ripoti hii inapendekeza kuwe na mafundisho kuhusu dawa za kulevya, athari zake na namna ya kuepuka matumizi yake katika mtaala wa elimu nchini Kenya.

**5.5 Uwanaharamu**

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, (2013) inaeleza kuwa, mwanaharamu ni mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa; mtoto aliyezaliwa na mama asiye na mume. Katika *Biblia Takatifu* kwenye kitabu cha Kumbukumbu za Torati (23:2)

> Mwanaharamu asiingie katika mkutano wa Bwana; hata kizazi chake cha kumi asiingie aliyewake katika mkutano wa Bwana.

Kulingana na *Biblia Takatifu*, mtoto aliyezaliwa kwa njia ya kukutana ndugu kwa ndugu au kuoana mtu wa Israeli na mtu wa mataifa au kuzaa na mke wa jirani yako au ambaye hamjaoana aliitwa mwana wa haramu au mwanaharamu. Mwana huyu hakuruhusiwa kuingia katika mkutano wa Bwana milele na hata kizazi chake.

Biblia inakataza kabisa jitihada zozote za kuzaa watoto nje ya muktadha wa ndoa. Kwanza Biblia inafundisha kwamba, tendo la uzazi limetengwa kwa ajili ya mume na mke katika muktadha wa ndoa. Kwa hivyo, jitihada zozote za kupata mimba nje ya ndoa ni dhambi. Sababu kuu ni kuwa inapigana na utaratibu uliowekwa na Mungu na ni uasherati. Dini inamhukumu mwana huyu. Inamfungia kuingia katika nyumba ya Bwana. Malezi ni jukumu la wazazi wote. Mpango wa Mungu kwa familia ni wazazi wawili, baba na mama, kulea watoto pamoja, na mpango huo lazima ubaki kuwa lengo la kila Mkristo.

Utamaduni wa jadi haukuruhusu mwanamke kupata mtoto nje ya ndoa. Makoti (2005) akimnukuu Mbiti (1969) anasema kuwa, utamaduni unapigwa vita na dini ya Kikristo na Kiislamu ili kuhakikisha umefifia. Makoti anahimiza

tuudumishe na kuthamini utamaduni wetu. Maoni ya Makoti yanaungwa mkono na utafiti huu, kwa kuwa utamaduni mwema unadhibiti maadili katika jamii. Kwa hivyo utamaduni ndicho kitovu cha maisha ya binadamu. Siku hizi kutokana na mabadiliko ya maisha na kukengeuka kwa wanajamii, kutokana na utamaduni wa kimagharibi, wanawake wameanza kupata watoto nje ya ndoa. Watoto hawa hukumbana na matatizo mengi hasa ikibainika kuwa watoto wa kiume hupenda kujitabulisha na ukoo wa kuumeni.

Katiba ya Kenya (2010), katika kifungu cha 53 (e) inampa kila mtoto haki ya asili ya malezi na ulinzi wa wazazi. Kifungu cha 53 (d) kinasisitiza kwamba maslahi ya mtoto ni muhimu katika masuala yoyote yanayomhusu. Sheria ya mtoto ya mwaka 2019, katika sehemu ya 4 na 8 inaangazia kanuni hii, ikiamuru kwamba ustawi wa mtoto lazima liwe jambo kuu katika makubaliano yoyote ya wazazi. Kulingana na maelezo haya, ni bayana kuwa kila mtoto ana haki ya kulindwa bila kubaguliwa.

Katika riwaya ya *Siku Njema*, mwandishi Ken Walibora amewasawiri wahusika wa kiume kama wanaharamu. Kongowea Mswawhili alikumbana na changamoto nyingi kutokana na uwanaharamu. Alipowashinda wanafunzi wenzake darasani, walisikika wakikengemeka. Wenye ushupavu na ushari walimbeua waziwazi bila kificho na kumwita 'kikojozi' au 'mwanaharamu.' Wanafunzi wengine kama Selemani walizoea kumwita mwanaharamu msi baba. Jambo hili lilimkera Kongowea sana. Mwandishi aneleza:

> Hili la kuitwa mwanaharamu lilinikera maini kama msumeno na kunikosesha furaha daima. (uk. 8)

Kutokana na nukuu hii, ni wazi kwamba kitendawili cha ni nani aliyekuwa baba wa mhusika Kongowea hakikuwa na wa kukitegua. Kongowea aliumizwa sana na kuitwa mwanaharamu. Kutokana na mamake kutoingia katika chuo chochote alipozaliwa aliitwa mwanaharamu. Kongowea aliamini kuwa hamna mwanaharamu; kitendo ndicho haramu. Taswira hii imetumika katika nukuu hii ili kuibua uzito wa matatizo wanayopitia wanaharamu katika jamii. Wanawake wanapouasi utamaduni huumiza kizazi cha kiume ambacho hupenda kujihusisha na ukoo wa baba.

Mawazo ya Kongowea Mswahili yanaungwa mkono na dini ya Kiislamu. Katika Uislamu kitendo hicho cha zinaa ambacho kimefanywa na mwanamume na mwanamke ndicho makosa na waliofanya wanafaa waadhibiwe hapa duniani ili wasafishwe kwa kosa lao hilo hadharani. Lakini tufahamu kwamba yule mtoto aliyezaliwa hana hatia yoyote. Allah asema hivi:

> "Na kila nafsi haichumii ila nafsi yake. Na habebi mwenye kubeba mzigo kwa Mola wenu. Naye atakuambieni mliyo kuwa mkitofautiana" (6:164)

Katika dini ya Kiislamu, haifai kwa Muislamu kumwita mtoto aliyezaliwa kwa jina mwanaharamu kwa sababu mtoto mwenyewe si wa haramu bali kitendo chenyewe ndicho haramu. Katika dini hii, mtoto aliyezaliwa kwa njia hii hataitwa kwa jina la huyu mwanamume aliyezini na mamake kwa sababu kisheria si mtoto wake. Utafiti huu unakubaliana na mawazo ya dini ya Kiislamu kwa sababu mtoto mwenyewe hana hatia.

Kongowea alikuwa na fikira nyingi kuhusu baba yake na ndipo aliamua kwenda kumsaka katika nchi ya Kenya. Alifikiria juu ya usuli wake na wazazi wake. Alikumbuka marehemu mamake, kalala kaburini usingizi usiojua wakati wa kuamka. Na baba? Ndipo alipoyatamka maneno haya:

> "Baba" kwangu lilionekana tu kama neno la Kiswahili lililoingizwa kwenye kamusi kwa makosa, halina maana. Halikuamsha katika moyo wangu hisia zozote za kutamanisha. Baba, baba nadharia tu ya wanafalsafa wenye makisio ya upuuzi. Macho yangu yalikuwa hayajawahi kumwona mtu wa kumwita baba. (uk. 69)

Kulingana na maneno ya mhusika huyu, neno baba halikuwa na maana kwake. Anamlaumu babake Juma Mukosi aliyesemekana yu hai na ambaye hakufaidi ulezi wake. Anajiuliza kwa nini mamake hakusubiri kumzaa katika heshima ya ndoa halali. Ijapokuwa kulingana na mhusika huyu jina baba halina maana kwake, ndani kwa ndani anaumia.

Japo ulimwengu unaendelea kukubali maisha ya kisasa, watoto wanaozaliwa nje ya ndoa hukumbana na madhila mengi. Wengi huwa na shida katika urithi, elimu, uchumba, uhusiano mwema na wanafamilia. Mtoto wa kiume wakati wowote uhusishwa na urithi. Mtoto haramu atokeapo katika familia maswali mengi huibuka. Atarithi shamba la nani? Akina ami humwona kama mzigo.

Vilevile, katika riwaya ya *Siku Njema*, mhusika wa kiume Rashid hakujulikana asili yake. Asili yake iligubikwa na giza totoro. Alijiona hana asili wala fasili. Mwandishi anaeleza haya:

> Marehemu mammake hakudiriki kumweleza lolote kuhusu usuli wake. Haikujulikana kama mama alitoka Uganda, Kenya wala Tanzania. Lililokuwa yakini ni kuwa hakuwa mwenyeji wa Mombasa Kisiwani. Alikuwa akiuza mboga na matunda katika soko la Mombasa Kisiwani, Alizaa mtoto

> mmoja tu, Rashid Omar. Rashid alikuwa miongoni mwa watu wanaoongezeka sana duniani ambao kuwauliza "baba yako ni nani?" ni kilele cha uchokozi mkubwa. (uk.71)

Kupitia nukuu hii ni wazi kwamba, kuuliza mtu baba yake ni nani kunaweza kusababisha fujo. Rashid hakumjua baba naye mama yake hakudiriki kumweleza, kwa hivyo baba kwake kilikuwa kitendawili. Mwandishi anaeleza kuwa Rashid alikuwa miongoni mwa watu wanaoongezeka sana duniani. Hili linaonesha kuwa wanaharamu wanazidi kuwa wengi duniani.

Wanawake wengi wanapopata watoto nje ya ndoa, wengi wao hukosa kuwaambia watoto wao baba zao ni akina nani. Wengine hudanganya kuwa baba yao alikufa. Watoto wanabaki bila kujua asili yao. Kwa heshima ya mwana kwa mzazi, wao huogopa kuwauliza mama zao baba ni nani. Akina mama wengi hujua asili ya mtoto, lakini kutokana na sababu kadha wa kadha huwaficha asili yao. Hili huchangiwa na hali kama vile mama huyu alipata mtoto kwa njia ya kuchuma, hivyo alilipwa. Kuna uwezekano kuwa mtoto aliyezaliwa alikuwa wa mume wa mtu mwingine, hivyo kuambiwa asili yake huenda akavunja ndoa ya mtu.

Uchumba wa Rashid ulipingwa sana na wazazi wa mchumba wake Zawadi kutokana na hali yake ya uwanaharamu. Hawakutaka mwana wao kuolewa na mtu asiyejulikana asili yake. Mwandishi anaeleza haya:

> Ndoa baina yake Zawadi na Rashid ni jambo ambalo wazee wake Zawadi hawakutaka litengenee Abadan. Kisa na maana ni kuwa Rashid alikuwa mwanamume asiyekuwa na asili wala fasili. Wazee wake Zawadi walijaribu kwa jino na ukucha kuhakikisha kuwa ndoa hiyo haikuwa. Suala la binti wao kuolewa na hadimu wa hoteli asiyejulikana jadi yake liliwakera maini wazee hao. (uk. 84)

Nukuu hii inaonesha jinsi mtoto ambaye hana asili hukumbana na changamoto maishani. Rashid alikuwa mwanamume mzuri aliyependwa na watu wengi. Wazazi wa Zawadi hawakumpenda, kisa na maana ni kuwa hawakujua asili yake. Walifurahia kifo cha Rashid. Walikuwa wamepanga kuleta rafu katika sherehe za harusi ya Rashid na Zawadi. Jambo hili lilipelekea Zawadi kula yamini kutorudi kwa wazazi wake tena.

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi,* suala la uwanaharamu linajitokeza. Mwandishi Clara Momanyi, anamtumia mhusika Mangwasha kuitambua jinsia ya kiume. Mangwasha amegundua kuwa kuna machache mno yanayomfunza mtoto wa kiume. Alitambua kuwa vijana wengi wa kiume hukumbana na mauti katika kujaribu kuwa wanaume. Katika jamii yake hakuna dira mahususi ya kumwongoza mtoto wa kiume. Nayo dira hiyo ni mzazi wa kiume. Haya yalimhuzunisha:

> "Ole wako ewe mwanamume uishiye leo. Unayechakura mapipa ili kuizima njaa. Ulikosea nini jamii hata usalie ombaomba? Umevaa koti kuukuu na umesalia kuwa nyuma kama koti hilo mwanetu. Yu wapi baba aliyekutelekeza? Iwapi jamii isiyothamini elimu yako? Jamii ilishika mkono mtoto wa kike. Ikasahau kwamba hata wewe unastahili kushikwa mkono. (uk. 138)

Kulingana na nukuu hii, mtoto wa kiume ametengwa na jamii. Mwandishi anauliza, yu wapi baba aliyekutelekeza. Mtoto anapotelekezwa na baba hubaki kuwa mwanaharamu. Mwanamume amekosa kumpa mwelekeo mtoto wake wa kiume. Mwandishi anammithilisha na dira. Mzazi wa kiume aliyemzaa na kumuacha bila wa kumwita baba. Mwanamume mpya hujali maslahi ya familia yake na kuitunza. Huwaelekeza watoto wake kama inavyostahili.

Mangwasha aliwaona pia wasichana wachanga na vitoto vyao mgogoni. Walipita kwenye barabara za miji, mikebe mikononi wakiomba wapita njia. Alifahamu kwamba vitoto hivyo vilizaliwa na wazazi wa kiume ambao pengine hata hawajulikani. Wapo lakini hawaonekani.

Katika jamii, wanaume husababisha uwanaharamu. Wanazaa watoto na kuwatelekeza. Watoto hawa hubakia mikononi mwa mama wasijue baba ni nani.

Katika habari za Tuko, Marchi 13, 2019, Jaji Njagi anasema kuwa, jukumu la uzazi linaashiria uwajibikaji kwa wazazi pindi tu mtoto anapozaliwa. Wazazi wa kiume hawawezi kuwa na uhuru wa kuyakubali au kuyakataa majukumu yanayotokea wakati mtoto anazaliwa. Jukumu la uzazi halifai kuamuliwa na mzazi mmoja awe baba au mama. Utafiti huu unakubaliana na mawazo ya Jaji huyu kwa sababu mwanamume mpya ana jukumu la kuipenda na kuilea familia yake.

Mapenzi ya kiholela baina ya wanafunzi wa kike na kiume katika vyuo vikuu huchangia uwanaharamu. Katika riwaya ya *Taswira za Mawingu*, mtoto Darlene alizaliwa kutokana na penzi la aina hiyo. Mhusika wa kiume Bramwel alipojua kuwa mpenzi wake Monii ni mjamzito, alikwepa majukumu ya ulezi na kumwacha Monii kushughulika na hali yake. Kinaya ni kuwa Bramwel alimhakikishia Monii kuwa daima yu naye lakini alipomaliza mtihani hakuonekana tena. Mwandishi anaeleza haya:

> Bramwel hatimaye alimaliza mtihani wake na akaondoka kuelekea kijijini kwao huku akimhakikishia Monii kwamba angerudi baada ya majuma matatu, kupiga kambi jijini na kusaka kibarua. Lakini baadaye mwezi mzima ulipita bila yeye kuonekana wala kuwasiliana. Na hatimaye miezi kadhaa ilipoyeyuka, Monii wasiwasi ukamwingia, moyoni ukamzagaa. Jitihada zake za kumpata kwa telegram, barua na hata kwa kutumia watu hazikufua dafu. (uk. 167)

Kulingana na maekezo haya, Bramwel hakuwa na mapenzi ya dhati. Hakuwa tayari kuwajibikia mtoto wake. Kule kukatiza mawasiliano na Monii ni bayana kuwa hakuwa tayari kwa ndoa. Matheka, (2014) anaeleza kuwa, baadhi ya sababu zinazowasukuma watu kuoa na kuolewa ni mbaya. Watu wengi wanajitosa katika ndoa kwa lengo la kuziridhisha tamaa za nafsi zao. Mapenzi ya dhati ni nadra katika jamii ya kisasa na mapenzi yasiyokuwa ya dhati yana misukumo mingi.

Mapenzi kati ya Monii na Bramwel hayakuwa ya dhati. Bramwel alitumia mapenzi kumuadaa Monii na kujinufaisha binafsi. Mtoto aliyezaliwa aliachwa mikononi mwa Monii na wazazi wake. Hii ni hali halisi katika jamii ambapo watoto wengi huachiwa nyanya na babu kama walezi. Idadi ya watoto wanaoachiwa nyanya na babu kama walezi inazidi kuongezeka. Katika Biblia kitabu cha Mhubiri, inaasema:

> "Mkumbuke Muumba wako siku za ujana wako kabla hazijaja siku
> zilizo mbaya" za uzeeni kwaweza kulemea. (12:1)

Wazazi wengi hawana nguvu za kukazia uangalifu wa kutosha watoto wadogo. Babu na nyanya pia wana jukumu la kuwatunza wazazi wao waliozeeka. Wazazi wengine hawana uwezo kifedha wa kutwaa mzigo huo. Kila mzazi anastahili kuwajibikia mtoto wake. Wengi wa wazazi hawa (nyanya na babu) wanasumbuliwa na aibu na hatia kwamba wameshindwa kufanikiwa wakiwa wazazi na wengi hujilaumu. Wengi hushangaa ni wapi walikosea wakiwa wazazi.

**5.6 Msongo wa Mawazo**

Msongo wa mawazo ni hisia ya kutoweza kukabiliana na mahitaji yanayotokana na kazi, mahusiano, shinikizo za kifedha na hali nyingine za maisha (Waeni, 2023). Ni kawaida kila mwanadamu kupata hisia za msongo wa mawazo, lakini zisiposhughulikiwa, zinaweza kuleta madhara makubwa kwa mhusika.

Wanaume wengi hukumbana na changamoto nyingi maishani. Bly (1990) anasema kuwa, kwa mwanamume sio jambo rahisi hasa anapotakiwa kutekeleza majukumu ya kijamii mbele ya macho ya umma. Kulingana naye, wanaume hukaa kimya na hukosa kuonesha dhalimu na matatizo wanayopitia. Hii ni kwa sababu katika jamii mwanamume hapaswi kuonesha unyonge wake. Wanaume hufanywa kama 'wafungwa' yaani wako na uhuru kimwili lakini wamefungwa na fikra zao, hali zao za kiuchumi, hisia zao na hata utamaduni wa jamii yake.Wapo watu wanaopoteza maisha kwa kushindwa kupata suluhu ya msongo wa mawazo. Wapo wanaotumia pombe, bangi na hata dawa za kulevya kujaribu kutibu hali hii.

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, mhusika wa kiume Bwana Sagilu, alikumbwa na msongo wa mawazo. Sagilu alishindwa na mpinzani wake katika Chama cha Mamlaka. Huyu alitia sahihi ya kumstaafisha kutoka katika safu ya siasa. Sagilu nazaa ilimvaa, mawazo yakamsonga kiasi cha kumtia kiwewe. Akili zikamruka. Mwandishi anaeleza haya:

> Sagilu alikuwa akiongea peke yake. Mara ainame na kubong'oa, mara apige makofi na kucheka peke yake. Alipobong'oa, watoto walimcheka huku wakimfuata na kumtania. (uk.146)

Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kuwa, Bwana Sagilu ana msongo wa mawazo. Alikuwa na matumaini makubwa ya kushinda katika uchaguzi wa chama chake. Mkewe alimtoroka na mwanawe kumkataa. Ni kawaida ya dunia hii kuchakaza watu kwa kadri wanavyoishi siku baada ya siku. Sagilu alipokuwa na mamlaka aliwatesa watu na kuwahujumu. Kweli wanaosema kabla hujafa hujaumbika hawakukosea.

Kutokana na maelezo haya, inabainika kuwa mabadiliko ya tabia ya Sagilu yanatokana na kufadhaika akili. Hali hii inadhihirika wakati Sagilu alipoonekana akipiga makofi na kucheka peke yake jambo lililowafanya watoto wamfuate wakimtania. Mwanadamu anastahili kujua kuwa matendo yake yanaweza kumwathiri mwenyewe. Ukitenda mema matokeo yatakuwa mema. Ukitenda mabaya matokeo yatakuwa mabaya.

Katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa*, Rashid anakumbwa na msongo wa mawazo alipopoteza kazi. Alipoisoma ile barua ya kufutwa kazi machozi yalimlengalenga. Aliamua kutomwambia mtu kuhusu hali yake. Kulingana na Farber (2020), kupoteza kazi maana yake ni kumalizika kwa mahusiano ya kikazi baina ya mwajiri na mwajiriwa. Kukatika kwa uhusiano huu kulimuumiza Rashid. Alipopigiwa simu na Karne alimweleza haya:

> "Kidogo. Kichwa kinaniuma. Hivi nilikuwa nimelala." "Kula *Asprin*, mpaka usiku utajiona hujambo. Nilitaka tuonane hivi leo usiku." "Sitoweza Karne, samahani. Kichwa kinaniuma na mazungumzo yako yananizidisha." (uk.205)

Kulingana na mazungumzo baina ya Rashid na Karne ni wazi kuwa, Karne hakujua kama Rashid kapoteza kazi. Rashid anaumwa na kichwa kutokana na mawazo mengi kuhusu kazi yake. Aliumika kisaikolojia. Kwa ajili ya mawazo mengi, alianza kuumwa na kichwa. Kuondoka kwake ofisini bila kumwambia yeyote kunaonesha kuumika ndani kwa ndani. Karne alimsaidia Rashid kupata suluhu la tatizo lake.

Katika riwaya ya *Siku Njema* mhusika wa kiume Mzee Kazikwisha alisongwa na mawazo alipokataliwa na Zainabu. Zainabu Makame alikuwa mamake Kongowea Mswahili. Bwana Kazikwisha alikuwa mhadhiri wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Alipokataliwa, maisha kwake yalikosa maana. Aliacha kazi yake na kuishi maisha ya ukiwa. Haya yanabainika katika kipande cha barua alichomwandikia mwanawe Kongowea:

> Mimi kweli wanifahamu? Kitovu changu ni Malindi. Nilikuwa Mhadhiri wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Mamako Zainabu Makame tulikutana zamani sana. Alikuwa mutribu aliyeghani nyimbo za taarabu kwa laani taamusi. Tulikutana Mombasa nilipokuwa nikitafiti lahaja ya Kimvita. Hatukusita kuchumbiana. Lakini maasidi walinifitini kwake Zainabu akanikataa. Kumbe nilikuwa nimefanya kosa la kumringa. Natubu na kumwomba Mwenyezi Mungu anighofirie madhambi yangu. Baada ya Zainabu kunikataa maisha yalikosa maana. (uk. 132)

Kutokana na nukuu hii, ni bayana kuwa Mzee Kazikwisha alikumbwa na msongo wa mawazo. Jina la kupanga walilompa wenyeji linaashiria mtu asiyekuwa na matumaini ya maisha. Alikataa kutangamana na watu. Watu nao walimwona kama mkia wa mbuzi na apizo kubwa. Watu wengine walisema kuwa alikuwa na kichaa. Aliishi katika ukiwa mkubwa. Watu walimwambaa kama mkoma.

Msongo wa mawazo humfanya mtu kuishi katika ulimwengu wake. Licha ya msongo wa mawazo kuwa kitu cha kawaida maishani mwetu, inaweza kuwa hatari isiposimamiwa vizuri. Ukiwa huu usipodhibitiwa unaweza kusababisha kifo au kurukwa na akili. Kukosa kufunulia mtu yeyote maisha yake kulimsababishia mzee Kazikwisha kifo cha ukiwa. Mwanawe Kongowea alipata mwili wake kitandani tayari umeoza na kunuka.

Mhusika wa kiume Kulesoni anakumbana na msongo wa mawazo katika riwaya ya *Taswira za Mawingu.* Baada ya kifo cha Kipsa mamake Kulesoni, maisha yalichukua mkondo mpya. Kulesoni alipitia mateso mengi mikononi mwa mama wa kambo Mwendi. Kulesoni alikuwa mwingi wa mawazo kuhusu mama yake. Alikuwa akifikiri kama amewahi kuishi, na umbo lake lilikuwa la aina gani. Kulesoni aliachwa na mama yake akiwa mtoto mdogo. Mwandishi anaeleza haya:

> Akiwaza akimwazia mtu anayempenda na kumhisi barabara akilini mwake ilhali hakuwahi kumwona hata mara moja. Hasha! Mtu ambaye daima yu moyoni mwake na nafsi yake imejifungamanisha naye. Na akili yake daima humkurubisha naye. Japo hayupo mtu huyu, kwenye nafsi yake yupo yaani tena sana. Mama yake. (uk. 2)

Kulesoni ana kumbukumbu za mamake mzazi. Anamhisi kwenye nafsi yake. Mawazo kuhusu mama yake yanadhihirisha kuwa kuna jambo fulani linalomsumbua. Mama wa kambo Mwendi alikuwa akimtesa na kumbagua. Alimfanyisha kazi nyingi na nzito huku wanawe wakiwa starehe. Alikuwa anaumwa sana na jino na mguu. Mwendi hakushughulika naye ila alimpa kazi ya kutafuta kuni majira ya usiku. Kulesoni anamlilia mama yake kwa kusema:

> 'Mama angekuwepo bila shaka angechemsha maji akaniosha na kunikanda mguu huu', Kulesoni aliwaza. 'Kisha angetwanga majani maalum akatia majimaji yake kwenye jani la mgomba na kuyatia joto motoni. Halafu angenisinga na bila shaka ningepata ahueni baada ya siku mbili au tatu.' (uk. 4)

Mawazo ya Kulesoni yanaonesha kovu la moyoni. Anatamani huduma ya mama mzazi lakini haikuwepo. Anamwazia mama yake ambaye hayupo duniani na mama wa kambo ambaye yupo ni afriti mkubwa, mbaya zaidi ya mauti. Watoto wa kiume wana ukuruba sana na mama mzazi. Wengi wanapoachwa na wazazi wao hukumbwa na msongo wa mawazo. Ni vizuri kwa walezi kuwa na moyo wa upendo wanapoachiwa watoto mayatima kuwatunza.

## HITIMISHO

Uchanganuzi uliofanywa ulidhihirisha kuwa wahusika wa kiume katika riwaya teule wanakabilianaa na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo ni kama vile dhuluma kutoka kwa jamii na walezi, kukosa kuendelea na masomo, hali ngumu ya maisha, uwanaharamu na msongo wa mawazo. Kuwakomboa wanaume kutokana na mila

zilizopitwa na wakati wanastahili kubadilika. Ikiwa mabadiliko yana manufaa hayafai kukataliwa. Mtafiti anapendekeza waandishi wa fasihi washughulikie changamoto za kila siku zinazowakumba wanajamii na kupendekeza njia mwafaka za kutatua changamoto hizo.